

## KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI

Dunia huadhimisha siku ya Kimataifa ya Usalama na Afya mahali pa kazi Aprili 28 ya kila mwaka ambapo Tanzania kama nchi mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) huungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hii. Kwahapa nchini, maadhimisho haya huratibiwa na OSHA kwa kushirikiana na wadau wengine wa utatu ambao ni Shirikisho la Vyama vyta Wafanyakazi (TUCTA) pamoja na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Kwa mwaka huu maadhimisho hayo yatafanyika Kitaifa Mkoani Arusha ambapo Kauli Mbiu ya maadhimisho ni: **Athari za mabadiliko ya tabia nchi katika usalama na afya kazini; Sajili eneo la kazi OSHA katika harakati za kupunguza athari hizo.**

OSHA imekuwa na desturi ya kuandaa na kutekeleza mpango maalum wa maadhimisho ambao hujumuisha shughuli mbali mbali zinazolenga kuendelea kuhamasisha uzingatiaji wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi hapa nchini. Katika maadhimisho ya mwaka huu, Wakala umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo;

- i. Maonesho ya Usalama na Afya mahali pa kazi yatakayo wakutanisha pamoja wadau wa maeneo ya kazi nchini kuonesha mifumo inayotumika kuwalinda wafanyakazi dhidi ya viharishi vya ajali, magonjwa na vifo mahali pa kazi ([Jisajili kushiriki maonesho](#))
- ii. Shindano la Tuzo za usalama na afya mahali pa kazi mionganoni mwa maeneo ya kazi yanayotekeliza vyema Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 ([Jisajili kushiriki shindano, pakua fomu ya tuzo](#)).
- iii. Bonanza la michezo litakalofanyika Aprili 26 Jijini Arusha katika uwanja ambao utatangazwa baadae ([Jaza taarifa za michezo ambayo Taasisi yako itashiriki](#)).

Hivyo, OSHA inapenda kualika Taasisi yako kushiriki katika shughuli zilizoainishwa ambazo zitafanyika kuanzia Aprili 23 hadi Aprili 30, 2024 Jijini Arusha.

## THE WORLD DAY FOR SAFETY AND HEALTH AT WORK 2024

Tanzania will join other countries across the world to commemorate the World Day for Safety and Health at Work on 28<sup>th</sup> April, 2024. This year's theme is; **The impacts of climate change on Occupational Safety and Health: Register workplace with OSHA in a move to reduce the impacts.**

At national level the commemorations will be held in Arusha Region. In marking the day, **OSHA** in collaboration with the **Association of Tanzania Employers (ATE)**, **Trade Union Congress of Tanzania (TUCTA)** and the **International Labour Organisation (ILO)** has arranged a number of Occupational Safety and Health promotion activities which include;

- i. Occupational Safety and Health exhibitions for employers and workers to showcase OSH Management systems used to protect workers against occupational accidents and diseases at their workplaces ([Download form to register to participate in the exhibitions](#)).
- ii. Awards for Occupational Safety and Health (AOSH) competition among workplace occupiers/employers who are effectively implementing the OSH Act, 2003 ([Apply for the AOSH-2024, download the application form](#)).
- iii. A sports bonanza on Friday 26<sup>th</sup> April to be held in Arusha at a location to be announced later ([Add details of sports your organization would like to participate](#)).

Therefore, OSHA has the pleasure to invite your organisation to participate in the mentioned activities which will take place starting from April 23<sup>rd</sup> to April 30<sup>th</sup>, 2024 in Arusha.